Mungu sawa sawa na neno liliandikwa '*mheshimu Bwana kwa mali yako na kwa malimbuko ya mazao yako yote; Mithali 3:9"*

Mungu amewabariki watu hawa kwa afya na vitu kama vile magari na ujuzi mbalimbali. Kwa jinsi ya pekee huduma hii imepata msaada mkubwa sana kutoka kwa *familia ya Mushi* ambao wametoa gari lao kutumika kwa ajili ya huduma. *Awali, haikuwa akilini mwangu kwamba tungekuwa tunatumia gari binafsi katika huduma hii. Nilifikiria kwamba tutakuwa tunatumia usafiri wa bus kisha tufikapo huko vijijini tungetumia usafiri wa aina yoyote ile ilimradi kutimiza kusudi letu*. Uhalisia ni kwamba tulipoanza kusafiri kwenda huko vijijni tuligundua kuwa kutokana na jiografia ya maeneo tunayotembelea, tusingeweza kufanya kazi hii kwa ufanisi endapo tusingekuwa na usafiri binafsi. Lakini kwa neema iliyo ya ajabu, familia ya Mr. Mushi ilibahatika kupata muujiza wa gari kubwa la hadhi ya aina yake siku chache tu kabla hatujaanza safari za mikoani.

Kwa bahati iliyo nzuri zaidi familia hii ikatoa gari lao kutumika kwa ajili ya huduma hii. Tumekuwa tukitumia gari hilo katika safari zetu za kubaini maeneo ya ujenzi na hata wakati wa kufuatilia hatua mbalimbali za ujenzi. Huko tunapotembelea, watu hudhani kuwa hilo ni gari la huduma na kwamba *Mr. Mushi ndiye dereva wa huduma. Siyo kweli kwamba hilo ni gari la huduma hii wala siyo kwamba Mr. Mushi ndiye dereva wa huduma hii bali ni kujitoa kwake.* Huku ni kujitoa kwa moyo mkuu sana kwa ajili ya kazi ya Bwana. Vile vile, wapo watu kati yetu ambao hawajawahi kukosa kuomba kwa ajili ya huduma hii, iwe kwa maombi ya pamoja au hata wakati wa maombi yao binafsi. Huu ni utajiri mkubwa wa watu ambao Mungu amewainua kwa ajili ya kazi yake.

Kwa jinsi ya pekee huduma hii imepata mchungaji mlezi wa huduma (*Mch. Joyce wa kanisa la TAG Nanjedya)* ambaye amekuwa na mzigo mkubwa sana wa maombi yeye na timu yake ya maombi wamekuwa msaada mkubwa sana. Wamekuwa wakifunga na kuomba kwa ajili ya huduma pamoja na kuombea mahitaji mbalimbali ya washirika wa huduma hii. Binafsi mchungaji huyu amekuwa msaada mkubwa sana kwangu kwani amesimama katika nafasi ambayo mimi binafsi kama Mkrugenzi wa huduma nisingeweza peke yangu kusimamia mambo yote haya.